JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 11- 2019/2020**

**DHIDI YA**

**LEROCK MEDIA GROUP**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**

## 1.0 Utangulizi

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa huduma za utangazaji kwa **Lerock Media Group,** kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mtandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yo yote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.3 Tarehe 22/02/2020 **Lerock Media Group** ilichapisha/iliweka mtandaoni kupitia Chaneli yake ya YouTube na mtandao wa Instagram ijulikanayo kwa jina la **"Simulizi na Sauti"** maudhui yenye lugha za matusi na yenye kushabikia vitendo vya ngono na unyanyasaji wa kijinsia.

1.4 **Lerock Media Group** ilitangaza habari hizo bila kuzingatia weledi, sheria, kanuni na maadili ya uandishi wa habari kwasababu mmiliki/mhariri wa Chaneli na Mitandao hiyo ya kijamii ijulikanayo kwa jina la **Simulizi na Sauti** aliweka/alichapisha picha jongefu ya mwanamke aliyejitambulisha kwa jina la **Zainab** akielezea visa vya watoto wadogo na vijana kufanyiwa ukatili wa kijinsia huko Bagamoyo.

1.5 Katika picha jongefu hiyo **Bi Zainab** alikuwa akielezea juu ya vitendo vya ngono na kulawitiwa kwa vijana na watoto katika Wilaya ya Bagamoyo na alionekana kufurahia na kushabikia vitendo hivyo jambo ambalo ni kinyume na maadili ya jamii ya Kitanzania.

1.6 Bi Zainab alisikika akizungumza maneno yafuatayo:-

***"mtoto mwenye miaka kumi na tatu, wana bakwa na kumwingilia mbele na nyuma, kwa sababu suala la kufanywa kinyume na maumbile hapa Bagamoyo ni kama Arabuni tu,...Bagamoyo kutoa mgongo kama vile Arabuni maana ukibakwa unatoa mgongo na mbele inakuwa nyongeza na nyuma kama kawaida..suala la kulawitiwa ni kama kawaida Bagamoyo ni Dubai tunaweza kusema...".***

***"...watu wanavua nguo kama walivyozaliwa uchi wanachezaa, watu kama hivyo wanalewa wanabakwa mbele na nyuma .... utasikia huyo kabakwaa, swala la kawaida mtu kaingiliwa mbele na nyuma watu eeeh!!! kamaliza mchezo huo Bagamoyo hiyo... mtaa unaitwaje? Nia Njema hiyoo! Utanyimwa vyote lakini sio mapenzi Bagamoyo... mwanmke hatongozwi, anashikwa tu mkono njoo twende zetu, shilingi ngapi, elfu kumi utakula mgongo nyuma nyongeza"***

## 2.0 Kanuni Zilizokiukwa

Kitendo cha kuweka maudhui hayo katika mitandao ya kijamii **Lerock Media Group** inatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 5(1) (a); (b); 5 (2) (b); 12 (a), (b), (d), (e), (f), (h) na (k)(i) za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni) 2018, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo;-

*5.-(1) For the purpose of these Regulations, an online content provider shall have the obligations to:-*

*(a) ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*

*(b) take into account trends and cultural sensitivities of the general public;*

*5 (2) A subscriber and user of online content services shall:*

*(b) ensure his posts do not contravene the provision of these Regulations and any other written law.*

*12: Online content services provider shall not publish: -*

*(a) indecent content saves for sex and nudity sex scenes approved by the body responsible for film censorship;*
*(b) Obscene content;*
*(e) sex crimes, rape or attempted rape and statutory rape, or bestiality;*
*(h) Content that causes annoyance, threatens harm or evil, encourages or incites crime, or leads to public disorder;*
*(k) content that uses bad language including-*

*(i) the use of disparaging or abusive words which is calculated to offend an individual or a group of persons*

## 3.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui

Tarehe 03 Machi, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia Uongozi wa **Lerock Media Group**, wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 12 Machi, 2020 saa 04:00 asubuhi, uongozi wa **Lerock Media Group** ukiongozwa na Bw. Fredrick Bundala, Mtendaji Mkuu na Mwanzilishi wa **Lerock Media Group** ambaye aliambatana na Bw. Escko Donald, Mtangazaji wa Vipindi, walifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao.

## 4.0 Kuangalia Maudhui ya Lerock Media Group

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Lerock Media Group** waliangalia maudhui mtandaoni ya tarehe 22 February, 2020 yaliyochapishwa katika chaneli zao mtandaoni ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au la.

## 5.0 Maelezo ya Utetezi ya Lerock Media Group

Uongozi wa **Lerock Media Group**, ukiongozwa na Bw Fredrick Bundala, ulitoa utetezi wao wa mdomo na pia ulikabidhi utetezi wa maandishi.

Katika utetezi wa maandishi na wa mdomo, Bw. Bundala aliiambia Kamati kuwa channeli yao ina vipindi mbali mbali, kikiwemo kipindi kiitwacho ***Kitaa Changu*** ambapo Mtangazaji huzunguka katika mitaa mbali mbali kujua furaha za watu na kero zao.

Waliendelea kuieleza Kamati kuwa katika kipindi kilichowekwa kwenye chaneli yao tarehe 22 February 2020 Mtangazaji alikuwa akiwahoji wakazi wa Bagamoyo hususani Mtaa wa Nia Njema kuhusiana na mambo wanayojivunia katika mtaa wao, ambapo wengi walizungumza sifa za mtaa huo, lakini mmoja wao aitwaye Zainab, yeye alieleza juu ya vitu asivyo vipenda katika mtaa huo anaoishi, ikiwemo michezo ya vigodoro ambavyo huchochea masuala ya ngono, ubakaji na ulawiti dhidi ya watoto na vijana.

Aidha, walisema kwamba katika mahojiano hayo kulikuwa na tatizo la matumizi ya lugha iliyokuwa inatolewa na Bi Zainab ambayo ilikuwa kali, na wao walijisahau kuihariri. Walikiri kosa, hivyo waliomba radhi.

Pamoja na utetezi wao wa maandishi, **Lerock Media Group** waliendelea kueleza yafuatayo:-

Bw. Fredrick Bundala, aliendelea kusema kuwa lugha iliyotumika ndiyo iliyokuwa kali kidogo, lakini yaliyozungumzwa ni mambo yenye ukweli, na hata wenyeji wa Mtaa husika walifurahi kuona tukio likitangazwa, kwani baadhi ya hatua zimekuwa zikichukuliwa na serikali ya Wilaya. Alisema baada ya kipindi kuonekana, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo alipiga

marufuku ngoma za vigodoro ambazo zilikuwa kichocheo kikubwa cha tabia hiyo mbaya.

Bw. Bundala aliendelea kusema, baada ya kipindi hicho kutangazwa wao waliitwa na Jeshi la Polisi Wilayani Bagamoyo kujieleza ni kwa nini hawakuwapa nafasi Polisi na viongozi wa Serikali kutolea maelezo hoja hizo zilizoibuliwa katika kipindi hicho.

Aidha, aliiambia Kamati kuwa wao pia wamechukua hatua kutokana na jambo hilo, ikiwamo kumrekodi **Bi Zainab** akiwa anaomba radhi kutokana na lugha aliyoitumia katika kipindi hicho, na wao pia wanaomba radhi kwa jambo hilo.

Vile vile, Bw. Bundala aliomba radhi kwa maandishi, na kuisihi Kamati kuwasamehe kwa sababu ni kosa lao la kwanza kwa kituo chao na kwamba wanaahidi kujirekebisha ili kutorudia kosa kama hilo. Alisema katika taarifa nyingi ambazo amezifanya hazijaleta shida yo yote na haikuwa lengo lake kutaka kuleta madhara katika jamii.

Kwa upande wake, Bw Escko Donald (ambaye ni mtangazaji wa kipindi hicho cha Kitaa Changu) alisema kwamba kituo chao kinatoa habari za kuburudisha, na vipindi vya aina hiyo alivyowahi kuvifanya sehemu nyingine havikuwahi kuleta madhara na wala haikuwa dhamira yao kutumia kipindi hicho kwa nia mbaya.

Bw. Escko Donald aliiambia Kamati kuwa yeye kucheka wakati akimhoji Bi Zainab ilimtokea kibinadamu na wala siyo kwamba alikuwa akifurahia maelezo ya Bi Zainab. Hivyo ameomba radhi kwani amegundua kuwa hakupaswa kuonyesha kama anafurahia jambo hilo.

Bw. Bundala alisema maudhui ya kipindi cha **Kitaa Changu** yapo katika mwelekeo wa kawaida ambao hauhitaji kuweka mizania ya habari. Aliongeza kusema kuwa tukio limewapa fundisho kuwa hata katika kipindi cha aina hii lazima kuwepo na uhariri ili kuweka mizania katika habari.

Katika kujumuisha utetezi wake, Bw. Bundala alisema maudhui ya Kipindi hicho yamewaumiza sana na wamelichukulia jambo kama hilo kuwa funzo katika utendaji wao.

Aidha alisema kuwa tangu wapewe Leseni na TCRA hawajawahi kukiuka Kanuni yo yote na kwamba wamekuwa wakifanya kazi zao kwa umakini na weledi mkubwa hivyo kosa hili liwe kama onyo na wasipewe adhabu.

Alihitimisha kwa kusema kuwa yeye kama mwanzilishi wa **Lerock Media Group, (simulizi na sauti)** ni kila kitu kwake kwani ndio nja pekee aliyonayo ya kumwingizia kipato.
Hivyo basi anarudia kuomba radhi kwa Kamati ili impe onyo pasipo adhabu nyingine, kwasababu hili ni kosa lao la kwanza na anaahidi kuwa **Lerock Media Group**, watakuwa waangalifu na kuzingatia weledi, maadili, sheria na Kanuni za utangazaji.

## 6.0 Tathmini ya Kamati

6.1 Baada ya kusikiliza utetezi wa **Lerock Media Group** Kamati imebaini kuwa licha ya kipindi kuibua masuala ya msingi na kero za wananchi wa Bagamoyo, kulikuwa na makosa katika kutangaza habari hiyo kutokana na lugha aliyotumia Bi Zainab. Aidha, takwimu zilizotolewa na Bi Zainab juu ya watu wanaofanyiwa vitendo vya ulawiti na ubakaji hazikuwa na udhibitisho kumeifanya habari hiyo kukosa mizania.

6.2 Kamati ya Maudhui imejiridhisha kuwa **Lerock Media Group** imefanya kosa kuchapisha na kutangaza maudhui ya matusi na yenye kushabikia vitendo vya ngono na unyanyasaji wa kijinsia kwa uzembe. **Lerock Media Group** ilitakiwa kuwa makini na kuzingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji.

6.3 Aidha kamati imebaini kuwa endapo **Lerock Media Group** wangezingati weledi maadili, sheria na Kanuni za Utangazaji ikiwa ni pamoja na kumwandaa Bi zainabu kabla ya kumhji habari hyo ingekuwa ni habari kubwa sana na ingesaidia kupata taarifa yenye uzito na mchang mkubwa kwa jamii na serikali na angekuwa amewatendea haki Wanachi wa wilaya ya Bagamoyo kwa kupaaza sauti juu ya kero hiyo.

6.4 Kamati imebaini kuwa **Lerock Media Group** ina tatizo la usimamizi na uhariri wa vipindi vyao kwasababu inaonekana kituo chao kinatatizo la kutokuwa na watu wenye elimu na weledi wa utangazaji.

6.5 Kamati imepokea taarifa ya hatua iliyochukuliwa na **Lerock Media Group** baada ya kosa kutendeka kwa kuondoa habari hiyo ili isiendelee kusambaa na mpango wao wa kuendelea kuwasiliana na Uongozi wa serikali ya Bagamoyo juu ya suala hilo. Kamati pia imepokea maelezo ya **Lerock Media Group** ya kuwaendeleza wafanyakazi wao kwa kuwapa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika Sheria, Kanuni, weledi na maadili ya uandishi wa habari.

6.6 Kamati imeridhishwa na ushirikiano waliouonesha **Lerock Media Group** wa kukiri kosa lao, kuomba radhi, na kuahidi kutorudia kosa.

## 7.0 Ushauri wa Kamati kwa Lerock Media Group.

7.1 Kamati ina lengo la kuimarisha tasnia ya habari na utangazaji nchini na kuwa haina nia ya kubana ubunifu wa watangazaji, bali inawataka wanahabari kuzingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa habari.

7.2 Kamati inatambuwa kuwa suala la utangazaji linahitaji watu wenye elimu bora, Maadili na Weledi katika tasnia ya Habari, hivyo **Lerock Media Group** inatakiwa kuwa na watangazaji wenye sifa hizo.

7.3 Hata hivyo kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Lerock Media Group** kuweka usimamizi thabiti wa habari na vipindi vyao ili kuhakiki na kuhariri maudhui yao kwa lengo la kujiridhisha kuwa yapo sahihi kisheria kabla ya kuyaweka mtandaoni.

## 8.0 Uamuzi wa Kamati

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Lerock Media Group**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Lerock Media Group** kupitia chaneli yake mtandaoni imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

**Hivyo Basi**, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu zifuatazo dhidi ya **Lerock Media Group;**

1. Kulipa faini ya **Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00)** tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mujibu wa Kanuni Na. 18 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018;

2. Kuomba radhi katika chaneli yao kwa muda wa **siku saba (7)** kuanzia tarehe 18 Machi 2020, kwa wananchi wa Wilaya ya Bagamoyo pamoja na wale wote ambao kwa namna moja au nyingine walikwazwa na habari hiyo.

3. Wanapewa Onyo.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo tarehe **17 Machi 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

Uamuzi huu umesainiwa na:

**Bw. Joseph Method Mapunda**

..............................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI WAFUATAO:**

**Bw. Abdul Ramadhani Ngarawa**..........................................

**Bw. Derek Kaitira Murusuri**..........................................

**Bw. Jacob Gregory Tesha**..........................................